

Mawakili Wa Serikali Watakiwa Kuongeza Kasi Ya Uwajibikaji

Mawakili wa Serikali Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wametakiwa kuongeza juhudni na uwajibikaji katika utendaji wao wa kazi ili kuiwakilisha vyema Serikali katika kusimamia, kushauri na kuendesha mashauri yanayoihusu Serikali na Taasisi zake.

Hayo yamesemwa na Wakili Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Gabriel Malata, alipoongea na watumishi wa OWMS ikiwa ni katika kuboresha utendaji kazi wa ofisi.

“Baadhi yetu tumeanza kufanya kazi chini ya kiwango na matokeo yake inakuja kuonekana hatumwakilishi ipasavyo Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa tunapokuwa mahakamani si kwamba tunaenda kuiwakilisha Ofisi bali tunaiwakilisha Serikali” amesema Malata

Malata amesema kuwa Ibara ya 35(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kuwa Shughuli zote za utendaji za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zitatekelezwa na watumishi wa Serikali kwa niaba ya Rais kwa maana hiyo OWMS imebeba dhamana ya kumwakilisha Mhe Rais na ndiyo maana mashauri yanafunguliwa dhidi ya Serikali.

Amewataka Mawakili wote wa Serikali kuendelea na kasi ambayo waliyokuwa nayo bila kurudi nyuma ili kuondoa malalamiko kutoka taasisi tunazoziwakilisha na kuwataka kuendelea kusimama kwenye nafasi zao kama tunavyotegemewa na Serikali katika kusimamia mashauri yake.

“Serikali inaendelea kuboresha maslahi ya watumishi na haitakuwa vyema kama Mawakili watafanya kazi chini ya kiwango hivyo tunapaswa kuongeza juhudni kwenye utendaji wa majukumu yetu na kama tunaona kuna changamoto zinazuia ari ya uwajibikaji msisite kuongea na uongozi kwa ajili ya kuzitatu” Alisema Mheshimiwa Malata.

Malata amewataka Mawakili kufanya maandalizi ya kina ya mashauri wanayokwenda kuiwakilisha Serikali au taasisi zake Mahakamani na kuhakikisha

kuwa wanaweka mawazo/ushauri wao kwenye mashauri hayo ili kuwasaidia Mawakili wengine pa kuanzia pindi atakapopata dharura.

Amewataka pia Mawakili hao kuhudhuria mahakamani katika mashauri yanayoendelea ili kukamilisha malengo ambayo ofisi imeingia na Serikali na kushindwa kufanya hivyo kutaondoa uhalali wa Mawakili hao kuwa ofisini na ofisi haitasita kuwachukulia hatua za kinidhamu kwa sababu wanaiondolea heshima OWMS.

Mheshimiwa Malata ametoa wito kwa Mawakili kuhakikisha wanaandikisha majibu ya mashauri yao mahakamani baada ya kumalizika kwa sababu suala hilo linagusa moyo wa majukumu ya ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Amesema yapao mashauri ambayo hayana majibu na yako mezani kwa baadhi ya Mawakili.

“Mawakili mnajua usipoandikisha majibu upande mwengine, wanapewa haki ya kusikilizwa bila upande mwengine kuwepo, ina maana hapo Serikali haitasikilizwa na shauri litaendelea bila Serikali na sisi Mawakili tupo,” alisema Mheshimiwa Malata.

Malata ameongeza kuwa ukiangalia maadili ya Mawakili wa Serikali yapo wazi kama yalivyoainishwa kwenye Gazeti la Serikali la mwaka 2019 namna gani ambavyo Mawakili wa Serikali wanatakiwa kutekeleza majukumu yao, hivyo Ofisi itasimamia kwa karibu kuhakikisha kila Wakili anatimiza majukumu yake.

Amewataka Mawakili kujibu nyaraka za upande mwengine ndani ya siku zisizopungua kumi na nne (14) tangu shauri mahakamani, kushindwa kufanya hivyo kunawakosesha haki ya kwenda kudhuria mahakamani na matokeo yake kuharibu kesi kwa mikono yao wenyewe.

Aidha, amewataka watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu kuendelea kuwa na ari ya kuipambania Serikali na kuwataka kutimiza wajibu wake kwa kujua madhumuni

ya kuwa katika OWMS na kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sharia, uwajibikaji na uadilifu na kuheshimu mgawanyo wa madaraka.

Naye Wakili wa Serikali Charles Mtae amemshukuru Wakili Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Malata kwa niaba ya watumishi na kusema watakwenda kuyatekeleza maagizo hayo kama alivyosema pamoja na kuongeza ari ya utendaji kazi kwa ujumla.